

## LIVING HOPE MINISTRIES-----2 WAKORINTHO 3

Paulo yuko na moyo wa ukweli juu ya wakristo wa Korintho. Anajua kwamba baadhi ya viongozi wako na maswali juu yake lakini tamannio lao ni kuwa wao wajue tumaini ambalo liko ndani ya Kristo na utukufu ulio ndani mwa Kristo.

### **Barua za kutambulisha**

Ni ya hekima kuwa na upambanusi juu ya watu wanao kuja kanisani, kwa sababu wengine wanaweza kuwa wa Baraka mbali wengine wanaweza kuwa waharibivu. Njia moja ya kuzaidia mwelekeo huu ulikukwa wa kuwa na barua kwa kanisa lingine. Lengo lilikuwa njema na lilikuzudia kulinda kanisa. Hata hivyo, wakati mwingine inaweza kuwa ya kujifunia au ya kuumiza. Paulo anahoji kuwa maisha yetu yanastahili kuwa barua na kuwa Roho wa Mungu anayefanya kazi ndani mwetu atatambulisha sisi kuwa tuko wa ukweli ndani mwa Kristo. Paulo hakuhitaji barua ya kumambulisha, kwa sababu maisha yake na huduma ulinena kwa nguvu juu ya uhusiano wake na Mungu. Alikuwa muhuduma aliye heshimika wa injili kwa sababu ya kazi ya Mungu katika maisha yake. Anasema kuwa yeye ni muhuduma wa Agano Jipya. Agano Jipya halibuuzi sharia ya Mungu lakini hafurahii katika neema ya Mungu, inayo maanisha kuwa tumekubalika ndani ya Kristo, hata kama hatufikii kiwango cha Mungu.

### **Agano Jipya**

Agano la kale lilikuwa limeandikwa kwa mawe, wakati Musa alipokea sharia Kumi na utukufu wa Mungu ulionekana kwa uso wa Musa. Huu ulikuwa ni wakati muhimu katika maisha ya Israeli, kwa sababu sharia kumi zilionyesha tabia ya Mungu na kiwango chake ambako kama watu wake wangemtii hizo sharia angewafanya wawe wa kipekee kutokana na mataifa mengine. Hii sharia ya haki pia ilionyesha jinsi moyo wa mwanadamu uliviokuwa wenye dhambi na jinsi tulivyo na hitaji kuu kwa ajili ya neema ya Mungu. Paulo anaandika juu ya Agano Jipya, ambalo linaleta haki na uhuru kutokana na dhambi. Utukufu ulio ng'aa kutoka kwa Yesu, unaweza pia kuangaza kutoka kwetu.

### **Nafasi yetu ndani mwa Kristo**

Tuko na Uwezo wa kuwa na tumaini kamilifu na kuwa wenye ujasiri mkubwa, kwa sababu ya kile ambako Yesu ametufanyia sisi. Tuko na Uwezo wa kuwa na uhusiana kibnafsi na Mungu. Tunaweza kuwa katika uwepo wake na hatuhitaji kitambaa cha kufunika uso wetu, kwa sababu Kristo anaondoa kila kizuizi ambacho kinaweza kututenga sisi na Mungu wetu. Roho wa Bwana ameguza roho zetu na kutuleta katika uhuru wa ajabu mbele ya Mungu. Tunajua kwamba sisi ni wenye dhambi lakini neema ya Mungu inamaanisha kuwa tunaweza ingia mbele ya uwepo wake na katika uwepo wake, tunabadilishwa na kuwa kama yeye. Utukufu wa muamini hauwezi kuja kutokana na juhudi zake au mpango wowote wa mwanadamu, mbali unatokana na Yesu mwenyewe-kile ambacho Paulo analeta ni kile kinacho badilisha maisha. Jinsi vile tunavyo zongea karibu na Yesu, ndivyo vile tunakuwa kama yeye na kwa hivyo, ndivyo watu wengine wanayoona Yesu ndani mwetu.

### **Vipengele vya kuzingatia**

1. Ni dhahadari gani wewe huchukuwa wakati unapo wakaribisha washirika wengine kanisani mwako?
2. Ni nini unacho hitaji ili kumpokea mtu kama mshirika wa kanisa lako?

3.Ni sehemu gani ambacho Agano la Kale lilifanya katika mpangilio au makusudi ya Mungu ili kutuleta sisi kwa Kristo?

4.Tunafurahia uhuru unao tokana na Agano Jipya kwa kiwango gani na tunawezaje kujizuia kutokuwa watu wa kufuatilia sharia?

5.Ni nini tunaweza fanya ili kupokea utukufu wa Mungu Zaidi katika maisha yetu,tukijua kuwa tutakapo fika mbinguni,utukufu utakuwa wa utele?

Mungu Akubariki

Richard Brunton